| 1. MRADI WA KUJENGA UWEZO WA KITAIFA KUWEZESHA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA<br>(Enhancing National Capacity for Implementation of the Environmental Management Act) | | |
|---|---|---|
| i. | Utangulizi | Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 imeweka mfumo wa kisheria na muundo wa kitaasisi kwa ajili ya usimamizi endelevu wa mazingira na maliasili nchini.<br><br>Sheria hii ilianza kutekelezwa 01 Julai, 2005. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Sheria hii ni pamoja na yafuatayo:<br>i) Kuanzishwa kwa Vitengo na Idara za usimamizi wa Mazingira katika Wizara za Kisekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa<br>ii) Kuandaliwa kwa Kanuni 16 na Miongozo 12 ya Usimamizi wa mazingira;<br>iii) Kuandaliwa kwa Mipango-kazi mitano (5) ya usimamizi wa Mazingira ya Wizara za Kisekta (Ujenzi; Maji; Kilimo; Afya; na Nishati na Madini);<br>iv) Kuandaliwa kwa mikakati mitano (5) ya usimamizi wa mazingira (Ardhi na Vyanzo vya Maji (2006); Bahari, Maziwa na Mabwawa (2008); Mabadiliko ya Tabianchi (2012-2018); Hifadhi ya Bioanuia (2015-2020); Viumbe Vamizi (2019-2030)); na<br>v) Mafunzo kuhusu sheria, kanuni na miongozo ya usimamizi wa mazingira pamoja na ukaguzi wa mazingira kwa Mamlaka za Usimamizi wa Mazingira (watu 300).<br><br>Hata hivyo, pamoja na juhudi mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali na wadau wengine, zipo changamoto katika utekelezaji wa Sheria hii ambazo ni pamoja na:<br>i) mchakato wa utoaji wa vibali vya mazingira kuchukua muda mrefu na hivyo kuathiri uwekezaji nchini;<br>ii) kutoandaliwa kwa baadhi ya Kanuni na miongozo ya usimamizi wa mazingira inayohitajika kwa ajili ya kuboresha hifadhi ya mazingira nchini;<br>iii) uwezo usiokidhi mahitaji wa taasisi zinazosimamia uzingatiaji wa Sheria;<br>iv) uelewa mdogo wa wadau kuhusu wajibu na majukumu yao katika utekelezaji wa Sheria husika; na<br>v) upatikanaji hafifu wa kanuni na miongozo ya usimamizi wa mazingira kwa ajili ya matumizi na wadau mbalimbali. |

| | | |
|---|---|---|
| | | Mradi huu ni wa miaka mitatu (3) (2020-2023) na unatekelezwa kwa gharama ya Shilingi Bilioni 6.9 (Dola za Marekani Milioni 3) kwa ufadhili wa Serikali ya Sweden. Mkataba wa Mradi ulisainiwa tarehe 31 Mei, 2020. Utekelezaji wa Mradi umeanza mwezi Oktoba, 2021.<br><br>Aidha, umefanyika kwa miaka mitano 2021-2026 |
| ii. | Lengo la mradi | Kuimarisha uwezo wa kitaasisi wa kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 |
| iii. | Malengo Mahsusi na Shughuli za Mradi | **Lengo Mahsusi #1: Kuimarisha mfumo wa kitaasisi na kisheria wa usimamizi wa mazingira** |

| | | Bajeti (USD) |
|---|---|---|
| 1.1 | Tathmini ya kina ya utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira tangu ilipoanza kufanya kazi | 80,000 |
| 1.2 | Kuandaa, kuchapisha na kutafsiri kwa Kiswahili Kanuni 15 za usimamizi wa mazingira | 600,000 |
| 1.3 | Kuandaa na kuchapisha miongozo 15 ya usimamizi wa mazingira | 300,000 |
| 1.4 | Kuandaa kanzidata ya sheria, kanuni, sheria ndogo na miongozo ya usimamizi wa mazingira | 10,000 |
| 1.5 | Kusaidia uanzishwaji wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Mazingira | 60,000 |
| 1.6 | Kutoa mafunzo na kununua vifaa vya kitaalamu kwa ajili ya Mamlaka za Usimamizi wa Mazingira | 200,000 |
| 1.7 | Kusaidia uanzishwaji wa Baraza la Rufaa la Mazingira | 25,000 |

**Lengo Mahsusi #2: Kuboresha mfumo wa utoaji vibali vya mazingira na mfumo wa ufuatiliaji**

| | | Bajeti (USD) |
|---|---|---|
| 2.1 | Kuboresha mfumo mtandao wa utoaji vibali vya mazingira | 70,000 |
| 2.2 | Kuanzisha kanzidata ya usimamizi wa taka nchini | 10,000 |
| 2.3 | Kuboresha mfumo mtandao wa tathmini na ufuatiliaji wa usimamizi wa mazingira | 50,000 |

**Lengo Mahsusi #3: Kuimarisha uwezo wa NEMC wa ufuatiliaji na usimamizi wa Sheria**

| | Bajeti (USD) |
|---|---|
| 3.1 Kununua maabara inayotembea *(mobile environmental laboratory)* | 300,000 |
| 3.2 Kununua vifaa vya kitaalamu vya kufanya uchunguzi wa haraka wa sampuli za mazingira *(field testing kits)* | 330,000 |

**Lengo Mahsusi #4: Kuboresha uwezo wa Wizara za Kisekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa Sheria**

| | Bajeti (USD) |
|---|---|
| 4.1 Kuandaa na kuchapisha Mkakati na Mpango-Kazi wa Taifa wa Usimamizi wa Taka | 90,000 |
| 4.2 Kutoa mafunzo kwa Mamlaka za Usimamizi wa Mazingira kuhusu nyenzo za usimamizi wa mazingira | 80,000 |
| 4.3 Kuandaa Mipango-Kazi ya Usimamizi wa Mazingira kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 2 (Jiji la Dodoma na Mji wa Njombe) | 100,000 |
| 4.4 Kutoa mafunzo kwa Wizara za Kisekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu tathmini ya mifumo ikolojia ya milima na kuandaa mipango-kai miwili (2) ya usimamizi na hifadhi ya mazingira | 40,000 |

**Lengo Mahsusi #5: Kuwezesha mawasiliano kwa umma na ushirikishwaji kimkakati wa wadau muhimu**

| | Bajeti (USD) |
|---|---|
| 5.1 Kuandaa Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano kwa Umma Kuhusu Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira | 40,000 |
| 5.2 Kununua vifaa vya kisasa kwa ajili ya Vitengo vya Mawasiliano kwa Umma vya OMR na NEMC | 100,000 |
| 5.3 Kuanzisha Kituo cha Taifa cha Taarifa za Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira | 85,000 |
| 5.4 Kuanzisha Jukwaa la Wadau wa Mazingira | 30,000 |

<table>
<tr><td></td><td></td><td>Lengo Mahsusi #6: Kuwezesha usimamizi wa Mradi
<table>
<tr><th></th><th>Bajeti (USD)</th></tr>
<tr><td>6.1 Kikao cha Uzinduzi wa Mradi na Kikao cha Mwisho cha Mradi</td><td>40,000</td></tr>
<tr><td>6.2 Kuendesha vikao vya Kamati ya Watalaamu na Kamati ya Usimamizi wa Mradi</td><td>120,000</td></tr>
<tr><td>6.3 Kununua vifaa vya ofisi kwa ajili ya OMR na NEMC</td><td>200,000</td></tr>
<tr><td>6.4 Tathmini na ufuatiliaji wa Mradi</td><td>50,000</td></tr>
<tr><td>6.5 Ukaguzi wa matumizi ya fedha za Mradi</td><td>30,000</td></tr>
</table></td></tr>
<tr><td>iv.</td><td>Bajeti</td><td>Shilingi Bilioni 6.9 (Dola za Marekani Milioni 3) kwa muda wa miaka 3 (2020-2023)<br><br>Kiasi cha Shilingi Bilioni 2.5 zimepokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi kwa mwaka wa kwanza</td></tr>
<tr><td>v.</td><td>Shughuli zilizotekelezwa</td><td>a) Kikao cha uzinduzi wa Mradi kilichofanyika tarehe 22 Aprili, 2021.<br>b) Kikao cha Kamati ya Wataalamu ya Usimamizi wa Mradi kilifanyika tarehe 16 Juni, 2021.<br>c) Kikao cha Kamati ya Usimamizi wa Mradi kilifanyika tarehe 21 Septemba 2021. Kikao hiki kiliidhinisha Mpango-Kazi wa Mwaka kwa gharama ya Shilingi bilioni 2.5.<br>d) Hadidu za rejea nne (4) zimeandaliwa kwa ajili ya tathmini ya utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira; kuandaa mfumo mtandao wa kutoa vibali vya Tathmini ya Kimkakati ya Mazingira na taka za kielektroniki; kuandaa Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Taka; na kuandaa Mpango-Kazi wa Usimamizi wa Mazingira wa Jiji la Dodoma<br>e) Ununuzi wa vifaa vya ofisi vya OMR uko katika hatua za mwisho (TZS milioni 311, ambapo hadi sasa Laptop 5 za manejimenti zimekwisha wailishwa na hadi kufikia tarehe 25 vifaa vilivyo baki vitawasilishwa.<br>f) Ukaguzi wa matumizi ya fedha za Mradi</td></tr>
<tr><td>vi.</td><td>Faida kwa jamii</td><td>a) Kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini kwa kupunguza muda wa utaoaji wa vibali vya mazingira;<br>b) Kuboresha nyenzo za kisera za usimamizi wa mazingira (kanuni, miongozo, mikakati na kanzidata) na hivyo kuchangia juhudi za hifadhi ya mazingira na kukuza uchumi;</td></tr>
</table>

| | | |
|---|---|---|
| | | c) kuimarisha ushirikishwaji wa wadau wa mazingira na hivyo kutoa fursa kwa makundi ya kijamii kuchangia na kunufaika na shughuli za hifadhi ya mazingira. |